

Ongeza mapato kutoka maua ya *Gladiolus*



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax. 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Magoti, R

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Embu

S.L.P27 Embu

Simu: 254068-31116/31873

Baruapepe: kariembu@salpha.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 35 /2008

Shilingi 20 za Kenya



Utangulizi

Ua la *Gladiolus* ni ua la thamani ambalo linaweza kukuzwa na wakulima wenye mashamba madogo ili kuimarisha mbinu za kujifaidisha kiuchumi.

Hunawiri mnapo mvua na huhitaji kunyunyiziwa wakati wa kiangazi.

Mahitaji ya kifedha ya kukuza ua hili si ghali ukilinganisha na maua yanayopandwa dani ya *green-house*.

Ukuzaji Wa Gladiolus

Vifaa vya kupunda

- Maua ya gladiolus hupandiliwa kutoka kwa *corms* na *cormels*.
- Chagua *corms* na *cormels* zilizo na afya na uzipande kiasi cha hamsini kwa kila mita jumla.

Nafasi ya mmea

Panda ukiacha nafasi ya sentimita 20 kati ya mistari na sentimita 10 kati ya mimea.

Mbolea

- Tia mbolea iliyokomaa kiasi cha kilo 10 kwa kila mita jumla na uongeze mbolea ya NPK kiasi cha gramu 50 kwa kila mita jumla
- Tia mbolea ya juu ya 17:17:17: N:P:K au mbolea ya CAN baada ya kila wiki mbili kiasi cha gramu 50 kwa kila mita jumla.
- Malisho ya matawi yanafaa kutiwa mwezi mmoja baada ya kupanda na utie baada ya kila wiki mbili hapo baadaye.

Ugezaji

Mbinu mwafaka ya kugezeza matawi mororo ni muhimu ili yakae wima. Unaweza kutumia vifaa vya chuma au miti.



Ugezaji ukitumia waya

Utunzaji mimea

Zuia wadudu wiki nne baada ya kupanda, kisha kila wiki mbili kabla ya maua kuchipuka.

Maradhi

Fusarium wilt, *bulb rot* na magonjwa ya kutu ndiyo magonjwa ambayo huathiri *gladiolus*. Tumia dawa za wadudu kama vile *brigade*, *benovap* au kopa *kocide* na kadhalika.



Kutu kwenye Gladiolus

Wadudu

Thrips, *aphids*, *mites* na *cutworms* huathiri *gladiolus* na dawa mwafaka ni lazima zitumiwe.

Kuvuna

- Vuna kwa kukata maua yaliyochipuka baada ya majani mawili ya kiini, wakati sehemu ya chini ya ua imeanza kuonyesha rangi.
- Tia mavuno kwenye ndoo ya maji na uhifadhi mahali pasipo na joto.



Wakati wa kuvuna

Maandalizi Ya Usafiraji

- Ili maua yasiegemea, tayarisha na usafirisha yakiwa yamesimama.

Kuinua

- Wiki mbili baada ya kuvuna, inua *corms* na *cormels* zikiwa kandokando. Tibu na dawa na uhifadhi kwenye baridi kwa muda wa wiki sita panapo ubaridi wa nyusi 2 hadi 40.